**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**SHULE YA WASICHANA NDWIKA** **S.L.P 427** **S.L.P 42**

**Simu:** 0714 996 141

**Barua pepe:** *ndwikagirlssecondaryschool@gmail.com*

---

**KUMB.NA.NDWK.J**1/1/2022 **06/04/2022.**

**Mzazi/Mlezi wa ..............................**

**S.L.P .............................................**

**Ndugu,**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI WASICHANA NDWIKA HALMASHAURI YA WILAYA MASASI MKOA WA MTWARA MWAKA 2022**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa binti yako ni mmoja kati ya wanafunzi wachache ambao wamebahatika kuingia kidato cha tano ili kuendelea na masomo ya sekondari. Binti yako amechaguliwa kujiunga kidato cha Tano mwaka 2022 katika tahasusi ya............ Katika shule hii ya sekondari ya wasichana Ndwika.

Kwa barua hii nakuleta fomu ya kujiunga na shule ya sekondari ya wasichana Ndwika. Tafadhali nakuomba wewe na mwanao msome maelekezo haya kwa kina na kisha mkamilishe yale yote yanayotakiwa.

Ni matarajio yangu kuwa baada ya kuikubali nafasi hii binti yako atafanya bidii katika masomo, na wewe kama Mzazi au Mlezi utashirikiana vema na shule kuhakikisha kuwa anaendelea hadi mwisho.

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana shule ya sekondari wasichana Ndwika.

Wako

Amina A Bakari

MKUU WA SHULE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**SHULE YA WASICHANA NDWIKA**
**S.L.P 427** **S.L.P 427-MASASI**

**Simu:** 0714 996 141

**Barua pepe:** ndwikagirlssecondaryschool@gmail.com

---

**KUMB.NA.NDWK/J1/1/2022** **06/04/2022.**
**MZAZI WA..............................**
**.....................................................**
Ndugu,

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA SHULE YA SEKONDARI WASICHANA NDWIKA MWAKA 2022**

**1. a) KUFUNGUA SHULE**

Muhula wamasomo utaanza tarehe ............. Kijana wako anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ............... na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe ................

**(b) MAHALI ILIPO SHULE**

Shule ya wasichana Ndwika ipo Mkoa wa Mtwara katika Wilaya ya Masasi, Tarafa ya Lulindi, Kata ya Lulindi, kijiji cha Ndwika chini, Km. 56 Mashariki mwa mji wa Masasi.

**(c) USAFIRI**

Wale watakao safiri kwa miguu na usafiri binafsi wafike Nagaga, barabara inayoelekea Newala ambapo-watafuata njia inayoelekea Kaskazini. Umbali kutoka Nagaga mpaka shuleni ni km. 6.
Kwa wale watokao Dar es salaam na mikoa mingine wapande mabasi yanayo kwenda masasi (sio mabasi yaendayo Mtwara mjini). Usafiri wa kufika shule (basi) unapatikana masasi stendi kuu (uliza magari yanayoenda **Newala** waambie wakushushe nagaga) au stendi ndogo ya TK, (uliza magari yaendayo **Newala**, na utateremka **Nagaga** au magari yanayoenda nagaga, ambapo utapata usafiri wakufika shuleni).

**MAELEZO/MAAGIZO NA MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA NDWIKA**

Mwanafunzi afikapo shuleni anatakiwa kuja na vitu vifuatavyo ambavyo vitakaguliwa na kukabidhiwa ofisini;

**1. AFYA**

i. Fomu (Medical Examination Results) imeambatanishwa. Ipelekwe Kwa Daktari wa Wilaya / Mkoa ili mwanafunzi akapimwe kuthibitisha afya yake. Tafadhali ijazwe kwa umakini na endapo mwanafunzi ana matatizo yoyote ya kiafya ambayo yanahitaji uangalifu wa pekee,

tafadhali tujulishwe mapema siku afikapo ili kujua namna ya kuweza kumsaidia awapo shuleni. Fomu hiyo irejeshwe shuleni siku ambayo mwanafunzi ataripoti na kusajiliwa

ii. **MUHIMU**, mwanafunzi ambaye hana bima ya afya anatakiwa kuja na kiasi cha Tsh 50,400/= kwa ajili ya kuandaliwa bima hiyo hapa shuleni. Fedha hii isiingizwe kwenye akaunti ya shule.

**2. URAIA**

Kabla binti yako hajafika shuleni itakubidi ujaze fomu (Affidavity) au alete cheti cha kuzaliwa kitakachothibitisha uraia wake. Fomu/Cheti hicho pia kirejeshwe shuleni wakati wa kuripoti na usajili wa mwanafunzi.

**3 ADA / KARO**

Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= za kitanzania kwa mwaka.Aidha anaruhusiwa kulipa shilingi 35,000 /= (yaani nusu ya ada ya shule) katika kila muhula. Ada ilipwe kupitia **AC. NDWIKA SEC SCHOOL RECURRENT A/C No.70501200112 NMB**, mwanafunzi anatakiwa aje na risiti ya benki (BPS) yenye jina kamili la mwanafunzi na sio mzazi au mlezi**'FEDHA TASILIMU HAZITA POKELEWA'**

**MICHANGO MINGINE NI KAMA IFUATAVYO**

(i) Tsh 5,000/ = kwa ajili ya tahadhari
(ii) Tsh 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
(iii) Tsh 15,000/= Ukarabati wa samani
(iv) Tsh 20,000/= kwa ajili ya taaluma.
(v) Tsh 30,000/= mchango wa ulinzi, wapishi na vibarua wengine
(vi) Tsh 2,000/= nembo ya shule
(vii) Tsh 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza.
(viii) Tsh. 20,000/= Mitihani ya kujipima (Joint)
(x) Tsh. 3000 Mchango wa umiseta.

**Jumla ya michango yote ni- 111,000/=**

Michango yote hii iwekwe kwenye akaunti ya **NDWIKA SELF-RELIANCE A/C. No.70501200172 NMB** .Aidha unaweza kutuma fedha ukiwa NMB TAWI LOLOTE **(ZINGATIA USICHANGANYE ADA NA MICHANGO KWENYE AKAUNTI MOJA)**

**4. MAHITAJI MENGINE:-**

Binti yako anatakiwa aje na yafuatayo shuleni.

A. **Sare ya shule**

i.Sketi 2 za Orange (rangi ya chungwa) ya kitambaa cha cotton ngumu na kizito (steem one) za mshono wa **V shape (linda mficho mbele)** Sketi ndefu inch moja kabla ya kongwa mbili (zinapatikana shuleni kwa bei ya tsh. 25000). **(Sketi fupi na inayobana hazitapokelewa).**

ii. Shati nyeupe mbili za mikono mirefu. Nusu kanzu mbili kwa wale wanaovaa hijabu. Na hijabu ni nyeupe.

iii. Viatu vya ngozi vyenye kamba jozi mbili, rangi nyeusi vyenye kisigino kifupi naViatu vyenye **visigino virefu na jamii ya buti havitaruhusiwa kabisa.**

iv. Soksi nyeupe jozi mbili.

v. Raba nyeupe Kwa ajili ya mazoezi na michezo.

vi. Bukta 2 rangi ya blue na sketi rangi ya **dark blue (bluu nyeusi)** mshono wa solo fupi kwa ajili ya michezo

vii. T-shirt nyekundu ya michezo yenye nembo ya shule (inapatikana shuleni Kwa Tsh 10,000/=)

viii. Sweta rangi ya kijivu lenye nembo ya shule (linapatikana shuleni Kwa Tsh 15,000/=)

ix. Magauni 2 rangi ya light blue (blue bahari) ambayo yatavaliwa wakati wa kazi za nje, ya **kitambaa cha cotton ngumu na kizito (steem one)** za mshono wa solo ndefu mpaka chini (gauni fupi hazitapokelewa).Kwa wale wanaova hijabu gauni liwe la mikono mirefu (Yanapatikana shuleni Kwa bei ya tsh. 30000 kwa moja)

x. Track-suti za rangi ya dark blue (blue nyeusi) kampuni ya Adidasi yenye mistari mieupe (isiyobana)

xi. T-shirt la shule lenye kola damu ya mzee (maroon) lenye nembo ya shule (linapatikana shuleni kwa Tsh 15,000/=)

xii. Neck-tai (Tai ndefu) ya rangi ya kitambaa cha sketi za darasani.

NB: Picha za mishono ya sare za shule imeambatanishwa kwenye fomu hii.

B. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anatakiwa kuja nayo

(i) Sanduku la chuma na begi moja la nguo

(ii) Daftali 12 @ 5000 (counter book quire 4 yanapatikana shuleni)

(iii) Godoro moja futi 2½ 16 (2½ kwa sita), yanakodishwa shuleni kwa Tsh.20, 000/= kwa mwaka. (Atalipa cash afikapo shuleni) / Pia anaweza kuja nalo.

(iv) Chandarua nyeupe (pembe nne)

(v) Shuka 2 za kulalia na kutandikia rangi ya pinki

(vi) Taulo moja na kandambili jozi moja.

(vii) Jembe 1 kubwa lenye mpini mrefu kwa kila mwanafunzi (yanapatikana shuleni kwa bei ya tsh. 10000)

(viii) Fagio la ndani 1, brush ya chooni ile fupi 1 na Kwanja 1 **(kwa wanafunzi wa CBG TU)** (kwanja linapatikana shuleni kwa bei ya tsh. 6000)

(ix) Reki 1na squeezer (skwiza ya kukaushia maji) 1.**Kwa wanafunzi Wanaochukua tahasusi ya HKL TU. (Reki** inapatikana shuleni kwa bei ya tsh. 10000)

(x) Brashi ngumu ya kusugulia sakafu yenye mpini mrefu 1, fagio ya kutolea buibui 1na panga 1.**Kwa wanafunzi wanao chukua tahasusi ya HGL TU** (panga linapatikana shuleni kwa bei ya tsh. 6000)

(xi) Ndoo 3 na galoni la lita 5 la kuifadhia maji ya kunywa.

(xii) Vifaa vya kulia chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

(xiii) Picha 'passport size' 4 za rangi katika sare/ uniform (shati jeupe lenye kola)

(xiv). Blanket 1 kwa wakati wa baridi

(xv). Mwanafunzi awe na nguo za ndani za kutosha na gagulo

(xvi) Mwanafunzi aje na toilet ball (toilet deodorant) na fagio la chelewa la nje moja.

(xvii) Mwanafunzi aje na graph pad moja (kwa wanafunzi wa **HGL & CBG**) na flat cover file 2 kwa wanafunzi wote

(xviii). Fedha za kutosha kwa matumizi yake ambayo ni muhimu, pamoja na fedha za kutumia awapo safarini ili asipate matatizo na vishawishi visivyo na lazima.**(mzazi mfungulie akaunti mtoto wako ambayo utakuwa unamtumia pesa ya matumizi kwenye bank ya NMB au CRDB Kwa sababu wakala wao wapo maeneo ya karibu na shule)**

(xvii) Ream za karatasi A4 **2 (Kwa mwaka)**
(xviii) Dissecting kit kwa wanafunzi wanaosoma Biolojia **(CBG) (ni lazima awe nayo kwa ajili ya kufanyia practical)**
(xix) Scientific calculator (CASIO function 991) Kwa wanafunzi wa masomo ya **sayansi na geography**.
(xx) Dawa ya chooni lita 1 aina ya **ARO** na sabuni ya unga **Doffi 1kg** kwa wanafunzi wa CBG
(xxi) **Sabuni za maji za kutengeneza lita 5** kwa wanafunzi wa tahasusi ya HGL & HKL
(xxii). Vitabu Angalia kiambata cha orodha ya vitabu.

**MWISHO**

**Pamoja na maelezo yote yaliyotangulia nakutumia:-**

(a) Nakala ya **SHERIA Na KANUNI** za shule. Tafadhali binti azisome na kuzielewa kwa uangalifu ili ziwe dira kwake na azifuate kama ilivyoelekezwa.

(b) Fomu ya kupimwa afya Hospitali (Medical Examination Results)

(c) Form ambayo mzazi ataijaza na kuweka na Picha nne za Wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu na mahali anapo ishi. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo na ni imani yangu kuwa utatekeleza yale yote tuliyoyaagiza kwa kikamilifu na uangalifu ili kutuondolea mimi na binti yako usumbufu usio wa lazima ikizingatiwa kwamba binti yako hawezi kupokelewa na kusajiliwa kuwa mwanafunzi wa shule hii bila kutekeleza maagizo yaliyotolewa.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya Mkuu wa Shule.........................

Jina la Mkuu wa Shule: Amina A Bakari

Muhuri wa Mkuu wa Shule.....................

*TUNAKUTAKIA MATAYARISHO MEMA NA MAFANIKIO*

**Namba ya simu mkuu wa shule: 0783 996 141**

**Namba ya simu ya makamu mkuu wa shule: 0711 668 455**

**Namba ya simu matroni: 0778 275 587**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.
SHULE YA WASICHANA NDWIKA
S.L.P 427 S.L.P 427-MASASI

**Simu:** 0714 996 141

**Barua pepe:** *ndwikagirlssecondaryschool@gmail.com*

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzisoma sheria na kanuni hizi kwa makini, azielewe na kuzishika au kuzifuata kwa utii wote. Hatua madhubuti na za kinidhamu zitachukuliwa bila kusita dhidi ya yule atakayekiuka.

**1) HESHIMA**

(i) Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kuwasalimu walimu au mtu yoyote aumri anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani kwenye ukumbi wa mikutano na mahali popote pale.

(ii) Mwanafunzi asitumie Lugha ya matusi au Lugha ya kihuni wakati wowote, mahali popote kwa wanafunzi wengine, kwa mwalimu au kwa mtu mwingine.

**NB:** Mwanafunzi haruhusiwi kutumia Lugha ya Kiswahili na au Lugha za asili akiwa darasani au nje, hasa wakati wa masomo badala yake atazungumza kwa Lugha ya kiingereza (Wakati wa kipindi cha Kiswahili na wakati mwingine utakaokuwa rasmi, Lugha ya Kiswahili kama lugha ya Taifa itatumika).Hii ni kwa sababu masomo yote katika shule za sekondari yanafundishwa kiingereza kama lugha ya kimataifa. Kanuni na sheria hii inawekwa ili kumjenga mwanafunzi uzoefu mkubwa wa kutumia lugha ya kiingereza na hivyo anaweza kuelewa sawasawa masomo yake na baada ya kuhitimu Elimu ya sekondari.

(iii)Uhusiano kati ya Mwalimu /Mfanyakazi na Mwanafunzi ni wa Mzazi na Mtoto. Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu Walimu na Wafanyakazi wote walioko shuleni kama Wazazi wake.

(iii) Mwanafunzi anapaswa kushirikiana na wenzake katika kazi, masomo na michezo n.k.

(iv) **Mwanafunzi haruhusiwi:-**

(a) Kuvuta sigara ya aina yoyote

(b) Kushiriki aina yoyote ya ulevi

(c) Kufuga kucha ndefu

(d) Kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi wala kunyoa tofauti na utaratibu mfano kunyoa kiduku

(e) Kupaka hina, rangi za kucha, wanja kunyoa nyusi na kujichubua ikiwa pamoja nakukalikiti nywele awapo shuleni.

(f) Kuvaa mavazi (sare za shule) yasiyo na heshima kubana, mavazi mafupi sana na yale yanayoonyesha umbile la mwili ndani ya mavazi.

(g) Kugombana na wenzake/mwenzake au na mtu mwingine yoyote.

(h) Mwanafunzi anapaswa kuheshimu Mali ya mtu binafsi na mali ya umma ikiwa ni pamoja na kutunza mali.
(i) Mwanafunzi anapaswa kufuata ratiba ya shule na masomo kikamilifu, ikiwa na kutii kengele na kuwahi katika shughuli zote za shule na mahali anapotakiwa kuwepo kila siku.
(j) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Serikali / Taifa, picha za viongozi mbalimbali. Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na wa Shule, pamoja na fedha za Taifa.
(k) Mwanafunzi anatakiwa kuwa mfano bora wa kuigwa na tabia / njema na heshima mahali popote ndani na nje ya shule.
(l) Mwanafunzi ashike na kufuata dini yake sawasawa.
(m) Mwanafunzi awapo darasani na katika mikutano anapaswa kunyoosha mkono juu anapouliza au kujibu swali / maswali.
(n) Mwanafunzi anatakiwa kutunza ukimya na awe maktaba wakati wa majifunzo ya usiku (Preparations).
(o) Mwanafunzi anapaswa kuwa msikivu wakati wa vipindi na asitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi.
(p) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kupokea tofauti za kisiasa, kidini, kiuchumi, na za kiutamaduni zilizopo katika jamii.

**2. MAHUDHURIO**

(i)Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shule kwa muda wote wa masomo.
(ii) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa
(iii) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria kazi zote za mikono
(v) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa, mikutano ya mabweni, mikutano ya darasa, mikutano ya vilabu vya masomo n.k.

**(3) MAANDALIZI YA JIONI**

(i) KILA Mwanafunzi atapangiwa bweni la kulala na kupewa kitanda.
(ii ) KILA Mwanafunzi atatakiwa kulala mahali alipopangiwa
(iii) Kutakuwepo na 'BED CHECKING' WAKATI WOWOTE wa usiku.
(iv) Mwanafunzi atalazimika kuhudhuria vipindi vya kujisomea usiku (prepo) kikamilifu.
(vi) Mwanafunzi atatakiwa awepo maktaba au darasani wakati wa prepo
(vii) Mwanafunzi haruhusiwi kulala bwenini wakati wa PREPO
(viii) Mwanafunzi anatakiwa kulala mara tu baada ya prep
(ix) Mwanafunzi ahakikishe anahudhuria 'Rollcal' wakati wowote

**(4) KUWAHI**

(i) Mwanafunzi anatakiwa kuwahi katika shughuli zote za Shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.
(ii) Mwanafunzi anatakiwa kuwahi anaposikia kengele ya wito wowote wa dharura
(iii) Mwanafunzi anataiwa kuripoti au kufika shuleni katika tarehe zilizopangwa Asichelewe au kuja tarehe nyingine.
(iv) Kengele ndiyo ishara ya mawasiliano kwa hiyo mwanafunzi anatakiwa kutekeleza wito wa kengele kutegemeana na ratiba ya shule na aina ya wito

**(5) MIPAKA YA SHULE.**

I. Ruhusa ya kwenda nje ya shule kwa matibabu itaidhinishwa na mwalimu wa zamu au matron baada ya mwanafunzi kufuata utaratibu uliopangwa wa kujaza fomu maalumu

II. Ruhusa ya kulala nje ya shule itaidhinishwa na mkuu wa shule baada ya mwanafunzi kufuata utaratibu uliopangwa wa kujaza fomu maalumu.

III. **Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa sababu maalumu.**

a) Chumba cha walimu.

b) Ofisi za walimu.

c) Maabara.

d) Jikoni.

e) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

f) Nje ya Shule.

g) Stoo ya shule

h) Nyumba za kulala wageni ('GUEST WING') za shule.

V. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule isipokuwa kwa ruhusa maalumu. Jumamosi/Jumapili ya Mwisho wa mwezi ataruhusiwa kutembelewa na ndugu, jamaa na marafiki wanaotambuliwa na shule na si vinginevyo.

VI. **Mwanafunzi haruhusiwi kamwe kutembelea sehemu zifuatazo:-**

a) Kwenye vilabu vya pombe.

b) Kwenye kumbi za starehe.

c) Kwenye nyumba ya kufikia wageni.

**(6) USAFI.**

I. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi kila wakati

II. Mwanafunzi atalazimika kufanya usafi katika mazingira ya shule kikamilifu

III. Mwanafunzi atalazimika :-

a) Kuhudumia kiwanja atakachopewa kukitunza

b) Kufanya usafi katika bwalo la chakula, bweni, darasa, vyoo, mabafu n.k

IV. Kutakuwa na ukaguzi wa usafi wa mara kwa mara.

V. Kutakuwa na mashindano ya usafi wa mabweni na madarasa.

VI Mwanafunzi hatoruhusiwa kusuka nywele awapo shuleni.

**(7) A. SARE YA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na sare ya shule iliyo safi na nadhifu wakati wote kama ifuatavyo:-

(i) Wakati wa Masomo darasani

(ii) Wakati wa kutoka nje ya Shule kwa shughuli maalumu za kishule.

(iii) Wakati wa Baraza la Shule.

(iv) Wakati wa kwenda Msikitini au Kanisani na Hospitali.

(v) Wakati wa Maandamano

(vi) Wakati wa kusafiri kuja shule au kwenda nyumbani kwa likizo. (Wakati wa likizo).

B. **Mwanafunzi wa kiislamu anaweza (kama anataka) kuwa na vazi la Hijab(nyeupe) kwa ajili ya sare ya shule.**

(i) Skirt ya orange

(ii) Nusu kanzu nyeupe ndefu yenye mikono mirefu kitambaa cha tetron.

(iii) Hijab nyeupe kitambaa cha tetron isiyokuwa na urembo wowote. **(Mavazi yenye rangi tofauti na sare ya shule hayataruhusiwa kamwe)**

**C. Gauni la kazi**

Wakati wa kazi za mikono au kazi za nje kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa gauni rasmi la kazi. Gauni la rangi ya light blue ndefu mpaka chini kwenye kongwa mbili. Hairuhusiwi kuvaa khanga au nguo ya aina yoyote isiyokuwepo kwenye sare ya shule, Gauni la kazi litavaliwa wakati wa kazi tu, na siyo darasani, msikitini, kanisani wala katika ukumbi wa mikutano au bwaloni. Asilete suruali, sketi za kubana au gauni ya aina yoyote wakati wote atakapokuwa shule atavaa sare za shule na gauni la kazi tu.

**D. Nguo za michezo**

Kila mwanafunzi awe na nguo za michezo ambazo atazitumia wakati wa michezo tu.Kama ilivyokwisha elekezwa nguo hizo zitakuwa fulana nyekundu, sketi ya blue inaweza kuwa fupi ili kuwezesha mwanafunzi kuruka, kukimbia na kujinyonganyonga kirahisi wakati wa kucheza. Raba nyeupe zitavaliwa wakati wa michezo kama sehemu ya sare.

## 8. UKUMBI WA CHAKULA (MESI)

(i) Chakula kitaandaliwa na wapishi wa shule katika jiko la shule

(ii) Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia chakula wakati wowote na mahali popote awapo shuleni

(iii) Chakula kitaliwa kwa kufuata ratiba isipokuwa kama itatokea dharura / tatizo lisiloweza kuzuilika na si vinginevyo

(iv) Chakula ni lazima kiliwe bwaloni tu na sio mahali pengine isipokua kwa wagonjwa waliolazwa na baada ya kufuata utaratibu na kupata ruhusa maalum.

(v) Mwanafunzi atakula chakula kitolewacho na shule kwa ajili ya wanafunzi wote si ruhusa kwa mwanafunzi kula magengeni au mitaani. Hii ni kwa sababu za kiusalama.

(vi) Shule HAINA UTARATIBU WA KUTOA MLO WA PEKEE ‘ SPECIAL DIET’ kwa mwanafunzi mwenye matatizo mbalimbali ya kiafya.

(vii) Mwanafunzi anatakiwa kufuata taratibu za kiungwana wakati wa kula, na anaruhusiwa kukibariki chakula chake kwa dini yake.

(viii) Hairuhusiwi kamwe kuingia na nguo chafu wala kuvaa kandambili / ndala katika bwalo la kulia chakula.

(ix) Mwanafunzi hatakiwi kupiga kelele wala kuzungumza na kucheka hovyo wakati wa kula hasa wakati wa matangazo na wakati wa kugawa barua kwa wanafunzi.

(x) Mwanafunzi ni lazima afanye usafi mahali anapolia chakula kila baada ya kula na kisha kusafisha vyombo vyake vya kulia chakula.

## 9. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHWA KUFUKUZWA SHULE

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi afukuzwe shule mara moja baada ya kuthibitishwa:-

(i) Wizi

(ii) Kupata mimba, kutoa mimba na kusababisha mimba

(iii) Uasherati , ushoga , ubakaji, na kushikwa ugoni

(iv) Ulevi, uvutaji wa bangi na sigara ikiwa ni pamoja na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile mirungi, cocaine, kubeli n.k.

(v) Kupigana na kupiga na makosa ya jinai

(vi) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa

ujumla
(vii) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
(viii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
(ix) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(x) Kumiliki au kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
(xi) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu na n.k
(xii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma na ya mtu binafsi ( kwa kosa hili mwanafunzi atafukuzwa baada ya kufidia uaribifu aliofanya)
(xiii) Kufuga ndevu
(xiv) Uvutaji wa sigara.
(xv) Kudharau Wimbo wa Taifa. Wimbo wa shule na Bendera ya Taifa.
(xvi) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja Kuolewa au kuoa
(xvii) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo, ikiwa ni pamoja na kukataa adhabu kwa makundi, na kuvuruga amani na usalama wa watu.
(xviii) Kushiriki au kuendeleza IMANI ZA KICHAWI / USHIRIKINA NA MAMBO YA MASHETANI hasa awapo shuleni.
(xix) Kukataa adhabu kwa makusudi
(xx) Mwanafunzi kumiliki simu ya mkononi akiwa shuleni
(xxi) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/Utoro

**10. MENGINEYO**

**AFYA:** (i) Mwanafunzi atalazimika kuhudhuria vipindi kikamilifu kutohudhuria masomo kwa ajili ya kuumwa mara kwa mara kutapelekea au kusababisha mwanafunzi huyo kusimamishwa masomo.
(i)Idhini ya mapumziko (ED) kwa ajili ya kuugua itatolewa na Mganga wa shule au Mganga wa Hospitali nyingine rasmi.Hivyo mwanafunzi asilete (sick bey) bila idhini ya Mganga na taarifa kwa Mwalimu wa zamu.

**MAWASILIANO**

(i) Lugha rasmi katika shule ya sekondari ni ya **KIINGEREZA** mwanafunzi atapaswa kuzingatia hili mara zote anapowasiliana na mwalimu yoyote au mwanafunzi mwenzake
(ii) Kiswahili kitatumika katika matukio rasmi na wakati wa kipindi cha Kiswahili (kama somo) au nje ya darasa.
(iii) Utoaji wa maoni ushauri na malalamiko utafuata ngazi na utaratibu uliopangwa k.m vikao vya bweni Baraza la shule uongozi wa wanafunzi na kadhalika
(iv) Kamwe, matusi, kashifa, kejeli, dharau na vurugu havitavumiliwa
(v) Barua za kiofisi za kwenda nje ya shule zitapitia na kudhibitishwa na Mkuu wa shule.

**UTENDAJI**

(i) Mwanafunzi atalazimika kutenda bila kusukumwa
(ii) Kazi zote zifanywe kwa ufanisi mzuri na kwa kiwango kinachotakiwa
(iii) Mwanafunzi atalazimika:
-Kuhudumia kiwanja atakachopewa (mazingira)
-Kuhudumia miradi ya shule (E. K)
- Kufanya usafi bwaloni, vyooni, bafuni n.k.
-Kufanya shughuli nyingine atakazopewa shuleni

- Kuhudumia mti mmoja wa matunda

**ULINZI NA USALAMA**

(i) Thamini na kutunza mali binafsi na ya umma/ shule

(ii) Mwanafunzi atalipia uharibifu au upotevu wa mali au kifaa chochote endapo atasababisha

(iii) Mwanafunzi atawajibika kwa kuwa na mgeni ambaye atatafutwa na polisi (serikali) au watu, baada ya kufanya kosa, uhalibifu wowote ule.

(iv) Kwa sababu yoyote mwanafunzi asihusishwe na kesi yoyote ya kimahakama bila taarifa kwa Mkuu wa shule.

(v) Mwanafunzi ni mpelelezi na mlinzi wa shule katika miaka yote ya uwanafunzi wake na lazima ashiriki kimamilifu katika usalama wa nchi na raia wake wote.

**KULALA**

(i) Mwanafunzi atalala katika bweni alilopangiwa.

(ii) Mwanafunzi atatakiwa kuwa kimya na kulala baada ya majifunzo ya usiku (PREP)

**(iii)** Ni kosa mwanafunzi kukosekana wakati wa **Bed checking, ROLL CALLS**

**MENGINEYO**

(i) Kanuni na sheria hizi sehemu tu ya taratibu njema za kuishi kwa amani na utulivu kwa lengo la kupata ufanisi kitaalamu na kitabia katika malezi ya mwanafunzi.

(ii) Walezi watakumbusha daima , kanuni na sheria hizi

(iii) Mwanafunzi ajitahidi kukosa makosa na kuepuka adhabu

(iv) Walimu ,Wafanyakazi , Wazazi na Walezi tushirikiane na kujenga Taifa lenye nidhamu kwa faida ya wote na Taifa letu

**(v) Mwanafunzi asije na simu wala kumiliki simu akiwa shuleni (SIMU ZIACHWE NYUMBANI).**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.
SHULE YA WASICHANA NDWIKA
S.L.P 427

**S.L.P 427-MASASI**

**Simu:** 0714 996 141

**Barua pepe:** *ndwikagirlssecondaryschool@gmail.com*

---

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA NDWIKA.**

**A: SEHEMU YA MWANAFUNZI:**

Mimi.......................................................Nakubali Kuingia kidato cha ...................................................katika shule ya wasichana Ndwika tarehe............................................................ Nitafika shuleni bila kuchelewa. Naahidi kwamba nitakuwa mwanafunzi bora mwenye bidii na utii muda wote nitakaokuwepo shuleni. Anuani yangu ya kudumu ni...........................................................................................

.....................

...........................................................................................

**SAINI YA MWANAFUNZI**.................................................................

**B. SEHEMU YA MZAZI**

Mimi.....................................................................Ninakubali/Sikubali Mtoto wangu....................................................... ajiunge na shule ya sekondari ya wasichana Ndwika Masasi kuanzia tarehe...................................... Naahidi kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kufika navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua. Ameahidi mbele yangu kwamba atakua mtiifu na mwenye bidii kazini na darasani. Mtoto wangu akiwa shuleni alelewe katika dini ya ..............................................

FOMU YA NDUGU WA WATAKAORUHUSIWA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI

| S\N | JINA, | UHUSIANO, | PICHA. |
|---|---|---|---|
| 1 | ........................................... | ...................... | |
| 2 | ........................................... | ....................... | |
| 3 | .......................................... | .... .................. | |
| 4 | .......................................... | ...................... | |

SAINI............................................................

Tafadhali fomu hii irudishwe shuleni kabla mtoto wako hajaondoka nyumbani au aje nayo siku ya kwanza anapokuja shuleni.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**SHULE YA WASICHANA NDWIKA**
**S.L.P 427** **S.L.P 427-MASASI**

**Simu:** 0714 996 141

**Barua pepe:** *ndwikagirlssecondaryschool@gmail.com*

---

KUMB.NA.NDWK................................................ **06/04/2022.**

Date........................
TO: Medical Officer,
Government Hospital,
.................................................
.................................................

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Name of Student .........................................................................
Please examine the above named student to her fitness as indicated below , and please arrange for necessary treatments so that the certificate may be signed and brought to school by the student. This certificate must be signed by a qualified Medical officer of a Government Hospital..
DATE........................................... SIGNATURE.............................

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above named student with regard to :-
Skin..................................................
Abdomen.................................
Eyes..................................................
stool.......................................
Fare...................................................
Urine......................................
Teeth.................................................. H/B
(Haemoglobin)........................
Chest.......................................................................................... ........
Any other disabilities.........................................................................
1. I consider that.............................................................(Name of student ) is in good health free from infection diseases , worms and fit to school.
2 .He/ she is fit to school after having treatmeant of................................
3 .She / He is not pregnant.........................................................................
4. Other comments (If any )..................................................................

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

DATE……………………………………………………………………………………

MEDICAL OFFICER.

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI**
**SHULE YA SEKONDARI NDWIKA**

**ORODHA YA VITABU**

**Na. SOMO JINA LA KITABU**

1. KISWAHILI ı Nadharia ya lugha Kiswahili 1 kidato cha 5& 6- J.A Masebo & ı Nadharia ya fasihi Kiswahili 2 kidato cha 5 & 6 –J.A Masebo

**USHAIRI**

ı *Kimbunga –Haji Gora*

ı *Mapenzi bora – Shaban Robart*

ı *Chungu Tamu – Theobald A. Mvungi*

ı *Fungate ya uhuru- Mohamed S. khatibhu*

***RIWAYA***

ı *Usiku utakapo kwisha – Mbunda Msokile*

ı *Kufikirika- Shabani Robart*

ı *Mfadhili – Hussein Tuwa*

ı *Vuta nkuvute- Shafi ADAM shafii*

***TAMTHILIYA***

ı *Kwenye ukingo wa thimu- Ebrahimu Hussein*

ı *Morani –Emanuel Mbogo*

ı *Kivuli kinaishi – Said Mohamed*

ı *Nguzo mama- Penina muhando*

2. GEOGRAPHY - Human and Economic Geography Advanced level. **D.T. Msabila**

Practical Geography – Zisti kamili

Physical Geography for Secondary Schools –**D.T. Msabila**

3. ENGLISH LANGUAGE

Advanced English practical approach – **Nicholas Asheli**

ı English form five and six – Oxford.

ı English Language for Secondary Schools Literature and Stylistics Form five and six.

ı I WILL MARRY WHEN I WANT-Ngug wa Thiong'i

ı LWANDA MAGERE- Okoiti Omtatah

ı A MAN OF THE PEOPLE-Chinua Achebe

ı AN ENEMY OF THE PEOPLE-Henrik Ibsen

4. BASIC APPLIED MATHEMATICS

ı Basic Applied Mathematics F5 &F6 (TIE B.I/2017)

5. HISTORY ı

HISTORY for secondary schools Form six (TIE)

Major Events- Mwijage
History one & two –Madaya
HISTORY for secondary schools Form five (TIE)
6. GENERAL STUDIES
**Richard R.F Mbalache** (2011) General studies for Advanced level certificate, Form five 1st editions. 3/2014
7 BIOLOGY ı\
BIOLOGY for Advanced level (1999) 4th Edition.- **Glannand Suzan Toole.** Nelson Thomes publisher. UK
ı BIOLOGICAL SCIENCE 3rd Edition Cambridge University press
ı Understanding Biology
8 CHEMISTRY
CONCEPTUAL CHEMISTRY Volume I, Chand. S. (2014**) New-Delhi S. Chand and Company PVT Ltd**.
Physical Chemistry – Advanced level.**Mark Daniel &HermersDamian,S**(2012)Dar –es salaam ,Ape Network.
Organic chemistry 1(part A
In organic Chemistry by Gary, L

**KIAMBATA CHA PICHA ZA MISHONO YA SARE ZA SHULE**





(a) Mfano wa shamba dress, mikono mirefu na mifupi (b) Mfano wa sketi ya shule inavyotakiwa.